

MKATABA MDOGO WA KUTUMIA ENEO

MKATABA HUU umetiwa saini leo hii tarehe. 29 mwezi wa 05 mwaka 2023.

KATI YA

TANZANIA ZHONGZHI AQUACULTURE COMPANY LIMITED WA S.L.P 646 MWANZA.(Ambaye kwenye mkataba huu ataitwa ‘Kampuni na MTUMIAJI WA SASA WA ENEO ALILOKODISHIWA’) na ambaye atashirikisha wadau na warithi wake kwa upande mmoja.

NA

QIRO GROUP COMPANY LIMITED SL.P 2226 ZANZIBAR(TIN NUMBER 142165066)(ambaye kwenye mkataba huu atajulikana kama Mtumiaji wa eneo) na ambaye atashirikisha wadau na warithi wake kwa upande mwingine.

Ifahamike kuwa huu ni mkataba mdogo, ni mkataba ambao umetiwa saini kwa mujibu wa kipengere cha 12 cha mkataba mama uliotiwa saini kati ya **TANZANIA ZHONGZHI AQUACULTURE COMPANY LIMITED WA S.L.P 646 MWANZA na TATU MASHIMBA** ambao unamtaka mkodishiwa wa eneo atoe taarifa kwa kwenye eneo kabla ya kumpa mtu mwingine eneo kwa ajili ya kulitumia,

Kwa kuwa kampuni ya **TANZANIA ZHONGZHI AQUACULTURE COMPANY LIMITED** inajishughulisha na shughuli za ufugaji wa samaki na kwa kuwa katika shughuli zake inakumbana na ugumu wa vyombo vya usafiri majini kama vile boti za faiba na kwa kuwa kampuni ya **QIRO GROUP COMPANY LIMITED SL.P 2226 ZANZIBAR** inajishughulisha na utengenezaji wa vyombo vya usafiri wa majini.



Handwritten signature or mark.

Hivyo basi Mkataba huu ni ushuhuda kuwa pande zote zimekubaliana hivi;

1.Kwamba,Kampuni **QIRO GROUP COMPANY LIMITED SL.P 2226 ZANZIBAR** itatumia eneo walilopewa na kampuni **TANZANIA ZHONGZHI AQUACULTURE COMPANY LIMITED** kwa muda wa miaka mitatu (03) kuanzia tarehe 29 mwezi 05 mwaka 2023 hadi tarehe 29 mwezi 05 2026.

2.Kwamba,kodi ya pango kwa mwaka inayolipwa kwa mwenye eneo(mwenye shamba) itaendelea kulipwa na kampuni ya **TANZANIA ZHONGZHI AQUACULTURE COMPANY LIMITED**.

3.Kwamba,kampuni ya **TANZANIA ZHONGZHI AQUACULTURE COMPANY LIMITED** haitakuwa na haki ya kuitumia kipande cha ardhi alichotoa kwa kampuni ya **QIRO GROUP COMPANY LIMITED SL.P 2226 ZANZIBAR** kwa muda wote ambao eneo hilo litakuwa linatumika na kampuni hiyo.

4.Kwamba, kampuni itawajibika katika kipindi chote cha mkataba kutunza mazingira ya eneo kwa kuzingatia taratibu ,kanuni na sheria za usafi wa mazingira.

5.Kwamba, mkataba huu utachukuliwa kuwa umefikia ukomo wake iwapo Kampuni kwa hiari yake yenyewe itaamua kuacha kuwa mtumiaji wa eneo husika na itawajibika kukabithi eneo hilo kwa kampuni ya **TANZANIA ZHONGZHI AQUACULTURE COMPANY LIMITED**.

6.Kwamba,baada ya miaka mitatu ya mkataba kampuni inaweza kuongeza tena muda wa mkataba wa kuendelea kutumia eneo hilo kwa masharti mapya.



[Handwritten signature]

7.Kwamba, mkataba huu unaweza kufanyiwa marekebisho muda wowote baada ya pande zote mbili kuwa na majadiliano na kukubaliana kwa maandishi juu ya mabadiliko ya Mkataba.

8.Kwamba kuvunjika kwa mkataba huu hakuzuii upande wowote uliopo katika mkataba huu kwenda mahakamani kudai haki yake.

Kwa ushuhuda huu pande zote mbili zinakubaliana kuwa makubaliano haya yatatekelezwa kwa kuzingatia sheria kuanzia tarehe ya leo kama inavyoonekana hapo juu.

Mkataba huu umesainiwa na pande zote mbili leo tarehe. 29.....mwezi.....05.....2023.

1.Kwa niaba ya kampuni ya **TANZANIA ZHONGZHI AQUACULTURE COMPANY LIMITED.**

Jina..... WANG WEI
Cheo..... Director
Saini..... 王偉
Tarehe..... 29 / 5 / 2023

2.SHAHIDI WA **TANZANIA ZHONGZHI AQUACULTURE COMPANY LIMITED.**

Jina..... MUSSA ELIAS MPANGO
Cheo..... FARM MANAGER
Saini..... [Signature]
Tarehe..... 29 / 5 / 2023



to

3. Kwa niaba ya kampuni ya **QIRO GROUP COMPANY LIMITED** kwa m

Jina..... YKUBU L/180
Cheo..... General Director
Saini..... J.K. V/S
Tarehe..... 29/05/2023



4. SHAHIDI WA KAMPUNI

Jina..... philipina costack mushi
Saini..... M
Cheo..... marketing manager
Tarehe..... 29/05/2023

MBELE YANGU

Jina..... Stephen M. Kaijage
Saini..... Mufungo
Wadhifa..... Commissioner for Oaths
Tarehe..... 15th June 2023



Handwritten mark or signature.